JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA

# Huduma zinazotolewa na PPAA

ppaa_tz

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| UTANGULIZI WA MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA (PPAA) | 1 |
| UAMUZI WA RUFAA DHIDI YA MAAMUZI YA AFISA MASUULI | 2 |
| UAMUZI WA RUFAA ZINAZOTOKANA NA KUFUNGIWA KWA WAZABUNI | 3 |
| UAMUZI JUU YA MALALAMIKO YATOKANAYO NA AFISA MASUULI KUSHINDWA KUTOA UAMUZI NDANI YA MUDA | 4 |
| UAMUZI JUU YA MALALAMIKO BAADA YA MKATABA WA UNUNUZI KUANZA KUTEKELEZWA | 5 |
| UAMUZI WA MAOMBI YA KUONGEZEWA MUDA WA KUWASILISHA RUFAA | 6 |
| UAMUZI WA MAOMBI YA KUKAZIA HUKUMU | 7 |
| UAMUZI MAOMBI YA KUFUTA UAMUZI ULIOTOLEWA KWA KUSIKILIZA SHAURI UPANDE MMOJA | 8 |
| UAMUZI WA  MAOMBI YA KUREJESHA RUFAA | 9 |
| MUHIMU | 10 |
| MAWASILIANO | 11 |

# UTANGULIZI WA MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA (PPAA)

Mamlaka ya Rufaa ni chombo huru kilichoanzishwa chini Kifungu 112 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya 2023. Lengo kuu la Mamlaka ya Rufani ni kuhakikisha migogoro ya ununuzi wa umma inatatuliwa kwa haki, uwazi, uwajibikaji na kwa muda mfupi.

---

# MAJUKUMU YA MAMLAKA YA RUFANI

### Mamlaka ya Rufani ina majukumu yafuatayo:

- ✓ Kupokea, kusikiliza, na kutoa maamuzi ya malalamiko au migogoro dhidi ya Taasisi Nunuzi ambapo mkataba wa ununuzi au uondoleaji mali tayari umeanza kutekelezwa.
- ✓ Kupokea, kusikiliza, na kutoa maamuzi ya rufaa zinazotokana na maamuzi ya kiutawala yaliyofanywa na Afisa Masuuli katika mchakato wa ununuzi
- ✓ Kupokea, kusikiliza, kutoa maamuzi ya rufaa zinazohusiana na kufungiwa kwa wazabuni kushiriki katika michakato ya ununuzi ya umma uliofanywa na PPRA.

---

# HUDUMA ZETU

### Mamlaka ya Rufaa hutoa huduma zifuatazo. Kwa kila huduma, maelezo yafuatayo yanatolewa:

- Uamuzi juu ya rufaa zinazotokana na mchakato wa ununuzi wa umma.
- Uamuzi juu ya rufaa zinazotokana na kufungiwa kushiriki katika michakato ya ununuzi wa umma.
- Uamuzi juu ya malalamiko yanayotokana na kushindwa kwa Afisa Masuuli kutoa uamuzi ndani ya muda uliowekwa.
- Uamuzi juu ya malalamiko baada ya mkataba wa ununuzi kuanza kutekelezwa.
- Uamuzi juu ya maombi ya kuongezewa muda wa kuwasilisha rufaa nje ya muda uliowekwa.
- Uamuzi juu ya maombi ya utekelezaji wa amri ya Mamlaka.
- Uamuzi juu ya maombi ya kufuta uamuzi uliotolewa bila kusikiliza upande mwingine (Ex Parte).
- Uamuzi juu ya maombi ya kurejesha rufaa.

# UAMUZI WA RUFAA DHIDI YA MAAMUZI YA AFISA MASUULI

## Maelezo:

Huduma hii inalenga kutoa uamuzi juu ya rufaa iliyowasilishwa na mzabuni ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa Afisa Masuuli.

## Nani Anaweza Kuomba?

**Mzabuni ambaye:**

- Aliwasilisha malalamiko kwa Afisa Masuuli; na
- Hajaridhishwa na uamuzi uliotolewa.

## Nyaraka Zinazohitajika:

- Fomu ya Rufaa Na.1
- Nakala ya uamuzi wa Afisa Masuuli
- Nyaraka za ushahidi zinazounga mkono rufaa

## Muda wa Kuwasilisha Rufaa:

Rufaa inapaswa kuwasilishwa ndani ya siku tano (5) za kazi tangu tarehe ya kupokea uamuzi wa Afisa Masuuli.

| Ada: | Muda wa Huduma: | Namna ya Kuwasilisha Maombi: |
|---|---|---|
| **TZS 500,000/=** | **Siku 40** | › Mfumo wa Kielektroniki wa (NeST – CAMM)<br>› Ofisi za PPAA - Dodoma<br>› Barua pepe Rasmi |

## MCHAKATO:

Kuwasilisha rufaa na nyaraka zake → Taasisi nunuzi kutoa majibu → Mapitio na uchambuzi wa shauri → Usikilizwaji wa Shauri → Maandalizi ya Uamuzi → Kutolewa kwa uamuzi

## Wajibu wa Mwombaji:

- Kujaza kikamilifu Fomu ya PPAA Na.1katika mfumo wa NeST.
- Kuambatisha nyaraka zote zinazohitajika.
- Kulipa ada ya huduma iliyowekwa.

## Haki ya Mapitio ya Kimahakama:

Mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa PPAA anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio ya kimahakama katika Mahakama Kuu ya Tanzania.

**KWA MAELEZO / MAWASILIANO ZAIDI**

Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA),
5 Mkandarasi Place, 58 Mtaa wa Lusinde,
S.L.P 1385, Dodoma, Tanzania,

+255 743 505 505
barua@ppaa.go.tz
www.ppaa.go.tz

# UAMUZI WA RUFAA ZINAZOTOKANA NA KUFUNGIWA KWA WAZABUNI

## Maelezo:

Huduma hii inalenga kutoa uamuzi juu ya rufaa iliyowasilishwa na mzabuni ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa kufungiwa kushiriki katika michakato ya ununuzi wa umma uliotolewa na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma ( PPRA ).

## Nani Anaweza Kuomba?

Mzabuni aliyefungiwa na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) na hajaridhishwa na uamuzi huo.

## Nyaraka Zinazohitajika:

- Fomu ya Rufaa Na.1
- Taarifa ya kufungiwa (Debarment Notice)
- Uamuzi wa kufungiwa
- Utetezi uliowasilishwa kwa Mamlaka(PPRA) kama upo.

## Muda wa Kuwasilisha Rufaa:

Rufaa inapaswa kuwasilishwa ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu kupokea uamuzi wa kufungiwa.

| Ada: | Muda wa Huduma: | Namna ya Kuwasilisha Maombi: |
|---|---|---|
| **TZS 500,000/=** | **Siku 40** | › Mfumo wa Kielektroniki wa (NeST – CAMM)<br>› Ofisi za PPAA - Dodoma<br>› Barua pepe Rasmi |

## MCHAKATO:

Kuwasilisha rufaa na nyaraka zake → PPRA kutoa majibu → Mapitio na uchambuzi wa shauri → Usikilizwaji wa Shauri → Maandalizi ya Uamuzi → Kutolewa kwa uamuzi

## Wajibu wa Mwombaji:

- Kujaza kikamilifu Fomu ya PPAA Na.1katika mfumo wa NeST.
- Kuambatisha nyaraka zote zinazohitajika.
- Kulipa ada ya huduma iliyowekwa.

## Haki ya Mapitio ya Kimahakama:

Mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa PPAA anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio ya kimahakama katika Mahakama Kuu ya Tanzania.

**KWA MAELEZO / MAWASILIANO ZAIDI**

Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA),
5 Mkandarasi Place, 58 Mtaa wa Lusinde,
S.L.P 1385, Dodoma, Tanzania,

+255 743 505 505
barua@ppaa.go.tz
www.ppaa.go.tz

# UAMUZI JUU YA MALALAMIKO YATOKANAYO NA AFISA MASUULI KUSHINDWA KUTOA UAMUZI NDANI YA MUDA

## Maelezo:

Huduma hii inalenga kutoa uamuzi juu ya malalamiko yanayotokana na kushindwa kwa Afisa Masuuli kutoa uamuzi ndani ya muda uliowekwa.

## Nani Anaweza Kuomba?

Mzabuni aliyewasilisha malalamiko kwa Afisa Masuuli na hakupokea majibu ndani ya muda wa siku 5 za kazi.

## Nyaraka Zinazohitajika:

- Fomu ya Malalamiko Na.1
- Nakala ya malalamiko yaliyowasilishwa kwa Afisa Masuuli

## Muda wa Kuwasilisha Rufaa:

Ndani ya siku tano (5) za kazi tangu siku ambayo Afisa Masuuli alipaswa kutoa uamuzi wake.

| Ada: | Muda wa Huduma: | Namna ya Kuwasilisha Maombi: |
|---|---|---|
| **TZS 500,000/=** | **Siku 40** | › Mfumo wa Kielektroniki wa (NeST – CAMM)<br>› Ofisi za PPAA - Dodoma<br>› Barua pepe Rasmi |

## MCHAKATO:

Kuwasilisha rufaa na nyaraka zake → Taasisi Nunuzi kutoa majibu → Mapitio na uchambuzi wa shauri → Usikilizwaji wa Shauri → Maandalizi ya Uamuzi → Kutolewa kwa uamuzi

## Wajibu wa Mwombaji:

- Kujaza kikamilifu Fomu ya PPAA Na.1katika mfumo wa NeST.
- Kuambatisha nyaraka zote zinazohitajika.
- Kulipa ada ya huduma iliyowekwa.

## Haki ya Mapitio ya Kimahakama:

Mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa PPAA anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio ya kimahakama katika Mahakama Kuu ya Tanzania.

**KWA MAELEZO / MAWASILIANO ZAIDI**

Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA),
5 Mkandarasi Place, 58 Mtaa wa Lusinde,
S.L.P 1385, Dodoma, Tanzania,
+255 743 505 505
barua@ppaa.go.tz
www.ppaa.go.tz

# UAMUZI JUU YA MALALAMIKO BAADA YA MKATABA WA UNUNUZI KUANZA KUTEKELEZWA

## Maelezo:

Huduma ya kushughulikia malalamiko pale ambapo mkataba wa ununuzi umeanza kutekelezwa.

## Nani Anaweza Kuomba?

Mzabuni aliyeshiriki katika mchakato wa ununuzi wa umma ambaye hakupokea notisi ya kusudio la kutoa tuzo na akafahamu kuwa mkataba wa ununuzi umeanza kutekelezwa.

## Nyaraka Zinazohitajika:

- Fomu ya Rufaa Na.1
- Nyaraka za ushahidi zinazounga mkono rufaa

## Muda wa Kuwasilisha Rufaa:

Malalamiko yawasilishwe ndani ya siku 5 tangu mzabuni afahamu utekelezaji wa mkataba.

| Ada: | Muda wa Huduma: | Namna ya Kuwasilisha Maombi: |
|---|---|---|
| **TZS 500,000/=** | **Siku 40** | › Mfumo wa Kielektroniki wa (NeST – CAMM)<br>› Ofisi za PPAA - Dodoma<br>› Barua pepe Rasmi |

## MCHAKATO:

Kuwasilisha rufaa na nyaraka zake → Taasisi Nunuzi kutoa majibu → Mapitio na uchambuzi wa shauri → Usikilizwaji wa Shauri → Maandalizi ya Uamuzi → Kutolewa kwa uamuzi

## Wajibu wa Mwombaji:

- Kujaza kikamilifu Fomu ya PPAA Na.1katika mfumo wa NeST.
- Kuambatisha nyaraka zote zinazohitajika.
- Kulipa ada ya huduma iliyowekwa.

## Haki ya Mapitio ya Kimahakama:

Mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa PPAA anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio ya kimahakama katika Mahakama Kuu ya Tanzania.

**KWA MAELEZO / MAWASILIANO ZAIDI**


Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA),
5 Mkandarasi Place, 58 Mtaa wa Lusinde,
S.L.P 1385, Dodoma, Tanzania,

+255 743 505 505
barua@ppaa.go.tz
www.ppaa.go.tz

# UAMUZI WA MAOMBI YA KUONGEZEWA MUDA WA KUWASILISHA RUFAA

## Maelezo:

Huduma hii inalenga kutoa uamuzi juu ya maombi ya kuongezewa muda wa kuwasilisha rufaa nje ya muda iwapo mzabuni alishindwa kuwasilisha rufaa yake kwa mujibu wa sheria.

## Nani Anaweza Kuomba?

Mzabuni ambaye:

- Aliwasilisha malalamiko kwa Afisa Masuuli.
- Hakuweza kuwasilisha rufaa ndani ya muda wa kisheria.
- Ana sababu za msingi zinazoeleweka kisheria za kuchelewa.

## Nyaraka Zinazohitajika:

- Fomu ya maombi Fomu Na. 2
- Nakala ya Malalamiko kwa Afisa Masuuli
- Uamuzi wa Afisa Masuuli
- Ushahidi unaoeleza sababu ya kuchelewa

## Muda wa Kuwasilisha Rufaa:

Maombi yanapaswa kuwasilishwa ndani ya siku tano (5) za kazi tangu tarehe ambayo alipaswa kuwasilisha Rufaa.

| Ada: | Muda wa Huduma: | Namna ya Kuwasilisha Maombi: |
|---|---|---|
| **TZS 1,000,000/=** | **Siku 40** | › Mfumo wa Kielektroniki wa (NeST – CAMM)<br>› Ofisi za PPAA - Dodoma<br>› Barua pepe Rasmi |

## MCHAKATO:

Kuwasilisha rufaa na nyaraka zake → Taasisi Nunuzi kutoa majibu → Mapitio na uchambuzi wa shauri → Usikilizwaji wa Shauri → Maandalizi ya Uamuzi → Kutolewa kwa uamuzi

## Wajibu wa Mwombaji:

- Kujaza kikamilifu Fomu ya PPAA Na.1katika mfumo wa NeST.
- Kuambatisha nyaraka zote zinazohitajika.
- Kulipa ada ya huduma iliyowekwa.

## Haki ya Mapitio ya Kimahakama:

Mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa PPAA anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio ya kimahakama katika Mahakama Kuu ya Tanzania.

**KWA MAELEZO / MAWASILIANO ZAIDI**

Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA),
5 Mkandarasi Place, 58 Mtaa wa Lusinde,
S.L.P 1385, Dodoma, Tanzania,
+255 743 505 505
barua@ppaa.go.tz
www.ppaa.go.tz

# UAMUZI WA MAOMBI YA KUKAZIA HUKUMU

## Maelezo:

Huduma hii inalenga kutoa uamuzi juu ya maombi ya kukazia hukumu yaliyowasilishwa na Mzabuni/Taasisi nunuzi kutokana na kutokutekelezwa kwa uamuzi uliotolewa na Mamlaka ya Rufani.

## Nani Anaweza Kuomba?

- Taasisi Nunuzi
- Mzabuni

## Nyaraka Zinazohitajika:

- PPAA fomu Na. 11
- Nakala ya amri au hukumu (decree/order)
- Uthibitisho wa kutotekelezwa kwa amri hiyo

## Muda wa Kuwasilisha Rufaa:

Maombi yanapaswa kuwasilishwa baada ya siku kumi na nne (14) kutoka tarehe ya uamuzi.

| Ada: | Muda wa Huduma: | Namna ya Kuwasilisha Maombi: |
|---|---|---|
| **TZS 1,000,000/=** | **Siku 40** | › Mfumo wa Kielektroniki wa (NeST – CAMM)<br>› Ofisi za PPAA - Dodoma<br>› Barua pepe Rasmi |

## MCHAKATO:

Kuwasilisha rufaa na nyaraka zake → Mapitio na uchambuzi wa shauri → Usikilizwaji wa Shauri → Maandalizi ya Uamuzi → Kutolewa kwa uamuzi

### Wajibu wa Mwombaji:

- Kujaza kikamilifu Fomu ya PPAA Na.11 katika mfumo wa NeST.
- Kuambatisha nyaraka zote zinazohitajika.
- Kulipa ada ya huduma iliyowekwa.

### Haki ya Mapitio ya Kimahakama:

Mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa PPAA anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio ya kimahakama katika Mahakama Kuu ya Tanzania.

**KWA MAELEZO / MAWASILIANO ZAIDI**

Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA),
5 Mkandarasi Place, 58 Mtaa wa Lusinde,
S.L.P 1385, Dodoma, Tanzania,

+255 743 505 505
barua@ppaa.go.tz
www.ppaa.go.tz

# UAMUZI MAOMBI YA KUFUTA UAMUZI ULIOTOLEWA KWA KUSIKILIZA SHAURI UPANDE MMOJA

## Maelezo:

Huduma hii inalenga kutoa uamuzi juu ya maombi yaliyowasilishwa na taasisi nunuzi ya kufuta uamuzi uliotelewa kwa kusikilizwa shauri upande mmoja (Ex parte decision).

## Nani Anaweza Kuomba?

Taasisi nunuzi ambayo ililalamikiwa katika rufaa na kushindwa kuwasilisa majibu ya rufaa au kufika katika usikilizwaji wa shauri na Mamlaka kutoa uamuzi uliosikilizwa upande mmoja.

## Nyaraka Zinazohitajika:

- Fomu ya maombi Fomu Na. 8
- Nakala ya Malalamiko kwa Afisa Masuuli
- Uamuzi wa Afisa Masuuli
- Ushahidi unaoeleza sababu ya kushindwa kufika katika usikilizwaji wa shauri

## Muda wa Kuwasilisha Rufaa:

Maombi yanapaswa kuwasilishwa ndani ya siku tano (5) kutoka tarehe ambayo uamuzi uliwasilishwa kwake.

| | Muda wa Huduma: | Namna ya Kuwasilisha Maombi: |
|---|---|---|
| **TZS 1,500,000/=** | **Siku 40** | › Mfumo wa Kielektroniki wa (NeST – CAMM)<br>› Ofisi za PPAA - Dodoma<br>› Barua pepe Rasmi |

## MCHAKATO:

Kuwasilisha rufaa na nyaraka zake → Taasisi Nunuzi kutoa majibu → Mapitio na uchambuzi wa shauri → Usikilizwaji wa Shauri → Maandalizi ya Uamuzi → Kutolewa kwa uamuzi

## Wajibu wa Mwombaji:

- Kujaza kikamilifu Fomu ya PPAA Na.8 katika mfumo wa NeST.
- Kuambatisha nyaraka zote zinazohitajika.
- Kulipa ada ya huduma iliyowekwa.

## Haki ya Mapitio ya Kimahakama:

Mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa PPAA anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio ya kimahakama katika Mahakama Kuu ya Tanzania.

**KWA MAELEZO / MAWASILIANO ZAIDI**

Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA),
5 Mkandarasi Place, 58 Mtaa wa Lusinde,
S.L.P 1385, Dodoma, Tanzania,

+255 743 505 505
barua@ppaa.go.tz
www.ppaa.go.tz

# UAMUZI WA MAOMBI YA KUREJESHA RUFAA

## Maelezo:

Huduma hii inalenga kutoa uamuzi juu ya maombi ya kuongezewa muda wa kuwasilisha rufaa nje ya muda iwapo mzabuni alishindwa kuwasilisha rufaa yake kwa mujibu wa sheria.

## Nani Anaweza Kuomba?

Mzabuni ambaye:

- Aliwasilisha malalamiko kwa Afisa Masuuli.
- Hakuweza kuwasilisha rufaa ndani ya muda wa kisheria.
- Ana sababu za msingi zinazoeleweka kisheria za kuchelewa.

## Nyaraka Zinazohitajika:

- Fomu ya maombi Fomu Na. 2
- Nakala ya Malalamiko kwa Afisa Masuuli
- Uamuzi wa Afisa Masuuli
- Ushahidi unaoeleza sababu ya kuchelewa

## Muda wa Kuwasilisha Rufaa:

Maombi yanapaswa kuwasilishwa ndani ya siku tano (5) za kazi tangu tarehe ambayo alipaswa kuwasilisha Rufaa.

| | Muda wa Huduma: | Namna ya Kuwasilisha Maombi: |
|---|---|---|
| **TZS 1,000,000/=** | **Siku 40** | › Mfumo wa Kielektroniki wa (NeST – CAMM)<br>› Ofisi za PPAA - Dodoma<br>› Barua pepe Rasmi |

## MCHAKATO:

Kuwasilisha rufaa na nyaraka zake → Taasisi Nunuzi kutoa majibu → Mapitio na uchambuzi wa shauri → Usikilizwaji wa Shauri → Maandalizi ya Uamuzi → Kutolewa kwa uamuzi

## Wajibu wa Mwombaji:

- Kujaza kikamilifu Fomu ya PPAA Na.2 katika mfumo wa NeST.
- Kuambatisha nyaraka zote zinazohitajika.
- Kulipa ada ya huduma iliyowekwa.

## Haki ya Mapitio ya Kimahakama:

Mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa PPAA anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio ya kimahakama katika Mahakama Kuu ya Tanzania.

**KWA MAELEZO / MAWASILIANO ZAIDI**


Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA),
5 Mkandarasi Place, 58 Mtaa wa Lusinde,
S.L.P 1385, Dodoma, Tanzania,

+255 743 505 505
barua@ppaa.go.tz
www.ppaa.go.tz

## MUHIMU

Zingatia muda uliowekwa wa kuwasilisha malalamiko, rufaa au maombi kwa Mamlaka ya Rufani
Mamlaka ya Rufani haishughulikii malalamiko yanayotokana na utekelezaji wa mkataba.

## HATUA ZA KUCHUKUA

Kwa maelezo zaidi au kuwasilisha rufaa, tafadhali tembelea tovuti yetu au wasiliana nasi moja kwa moja. Tupo tayari kukuhudumia na kuhakikisha mchakato wa ununuzi wa umma wenye haki, uwajibikaji na uwazi.

## HITIMISHO

Kipeperushi hiki kinatoa muhtasari wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Majukumu yake, na huduma inazotoa chini ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya mwaka 2023. Tumejizatiti kuhakikisha haki, uwazi na uwajibikaji katika utatuzi wa migogoro ya ununuzi wa umma. Wasiliana nasi kwa maelezo zaidi na mwongozo.

**KWA MAELEZO / MAWASILIANO ZAIDI**


Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA),
5 Mkandarasi Place, 58 Mtaa wa Lusinde,
S.L.P 1385, Dodoma, Tanzania,

+255 743 505 505
barua@ppaa.go.tz
www.ppaa.go.tz

PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY

Efficient and Fair Appeals Dispensation

PPAA

MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA)**
**5 Mkandarasi Place,Ghorofa ya nne, 58 Mtaa wa Lusinde,**
**S.L.P: 1385 Dodoma, Simu: +255 743 505 505,**
**Piga Bure: +255 262 962 411, Barua pepe: es@ppaa.go.tz**
**Website : www.ppaa.go.tz**

**ppaa_tz**